## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI SEPTEMBA, 2023 NA MWELEKEO KWA MWEZI OKTOBA, 2023.

**Dondoo za tathmini ya Septemba, 2023 na mwelekeo wa Oktoba, 2023:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Septemba, 2023 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Oktoba, 2023 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2023 hali ya ukavu iliendelea kujitokeza katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, vipindi vichache vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani, nyanda za juu kaskazini mashariki, ukanda wa ziwa Victoria na maeneo ya magharibi mwa nchi. Aidha, vipindi vya baridi vilijitokeza katika maeneo machache hususani nyanda za juu kusini magharibi.
ii. Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2023, mvua za Vuli zinatarajiwa kuanza katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, ongezeko kidogo la joto linatarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2023.

Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2023 hali ya ukavu iliendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi, pamoja na vipindi vya baridi hususan nyakati za usiku katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi. Viwango vya chini zaidi vya joto kati ya nyuzi joto 7 °C na 14 °C viliripotiwa katika maeneo ya Igeri (Njombe) na Uyole (Mbeya). Aidha, viwango vya joto la juu viliongezeka kidogo katika maeneo mengi ya nchi. Mnamo tarehe 29 Septemba,2023 kituo cha Mpanda kiliripoti kiwango cha juu cha nyuzi joto 35.2 °C. Kwa upande mwingine, vipindi vichache vya mvua viliripotiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani, nyanda za juu kaskazini mashariki, ukanda wa ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 45.7

kilipimwa katika kituo cha hali ya hewa Same (mkoa wa Kilimanjaro) mnamo tarehe 29 Septemba,2023. Aidha, katika kipindi hiki vipindi vifupi vya upepo mkali unaofikia kasi ya km 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan ukanda wa pwani na mkoa wa Songwe.

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI OKTOBA, 2023

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2023 joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la juu ya wastani, ikiashiria uwepo wa hali ya El Niño. Aidha, joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuendelea kuwa juu ya wastani, na eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi chini ya wastani. Hali hii inatarajiwa kusababisha uwepo wa upepo wenye unyevu unaovuma kuelekea ukanda wa pwani pamoja na maeneo jirani ya pwani. Katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola), hali ya joto la bahari la wastani inatarajiwa kuendelea. Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango hafifu wa kusababisha upepo wenye unyevu kutoka misitu ya Congo kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Hata hivyo, joto la bahari la juu ya wastani katika ncha ya kusini mwa Afrika linatarajiwa kuendelea na hivyo kupunguza uwepo wa hewa yenye ubaridi kutoka kusini na kusababisha ongezeko la joto katika baadhi ya maeneo nchini. Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa Afrika inatarajiwa kupungua nguvu kiasi na kupelekea Ukanda mvua (ITCZ) kuanza kusogea kuelekea kusini.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2023

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2023, mvua za msimu wa Vuli zinatarajiwa kuanza katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, kuna uwezekano wa ongezeko la mvua kwa baadhi ya maeneo katika wiki ya tatu na ya nne. Kwa upande mwingine, hali ya joto kiasi inatarajiwa hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu na ya nne.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Katika kipindi hiki, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu na ya nne.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua vinavyoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Oktoba,2023.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Kiujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi, Aidha, vipindi vichache vya mvua vinaweza kujitokeza katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. Aidha, vipindi vya baridi vinatarajiwa kuendelea kujitokeza hususan katika maeneo ya miinuko.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani. Aidha ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya nne ya mwezi.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. Aidha ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya nne ya mwezi.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI NOVEMBA, 2023

Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2023 vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi nchini. Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo.

## 2.4 USHAURI

Mvua za Vuli, 2023 zinatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2023 katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza, hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zitakazojitokeza..

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Oktoba, 2023 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz